

# Siku ya Ubatizo Wangu



**Na Megan S., umri miaka 10,  
Michoacán, Mexico**

Habari! Jina langu ni Mergan, na ninaishi Mexico. Ninataka kukuambia kuhusu wakati maalumu sana katika maisha yangu—siku niliyobatizwa.



Nilipatizwa kwenye siku yangu ya miaka nane ya kuzaliwa. Ilikuwa siku yangu muhimu sana kwa sababu nilisherehekea siku ya kuzaliwa kwangu kwa kubatizwa.

Kubatizwa lilikuwa tukio zuri sana. Mama yangu alinitengeneza daftari lenye shughuli tofauti tofauti ili kujandaa. Lilinisaidia mimi kujifunza kuhusu umuhimu wa ubatizo na maagano ambayo ningefanya na Baba wa Mbinguni.



VIELEZO NA OLGA LEE

Watu wengi wanaonipenda walikuja kwenye ubatizo wangu. Nilihisi furaha sana kwamba walikuja. Nilivaa gauni jeupe, na maji yalikuwa ya uvuguvugu.



Daima nitaikumbuka siku ile. Ilikuwa maalumu sana kwa sababu nilifanya agano langu la kwanza na Mungu. Niliahidi kumfuata Yesu na kutii amri Zake.

Kama una wasiwasi kuhusu siku yako ya ubatizo itakuwaje, usihofu. Baba wa Mbinguni ataka wa furaha kuhusu uchaguzi uliofanya. ●



Baada ya baba yangu kunibatiza, nilijikausha na kubadilisha nguo. Kisha nikapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Nilithibitishwa kuwa muumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho na wenyewe ukuhani. Nilijihisi mwenye amani, upendo na furaha tele.